

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI



TANGAZO KWA WATUMISHI WA UMMA TAREHE 17/03/2025

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI ANAWATANGAZIA WATUMISHI WOTE KUWA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KUPITIA REKEBISHO LA WARAKA NA C. WA WATUMISHI WA SERIKALI NA. 3 WA MWAKA 2012 KUHUSU UTARATIBU WA KUKOPESHA FEDHA TASLIM WATUMISHI WA SERIKALI KWA AJILI YA KUNUNUA MAGARI, SAMANI NA MATENGENEZO YA MAGARI NA PIKIPIKI KWA RIBA YA ASILIMIA 4 KWA UTARATIBU UFUATAO: -


A. Ukopeshaji wa fedha Taslim

- ✓ Mkopo utazingatia kiwango kulingana na ngazi ya Mshahara wa Watumishi na awe na Salio la **1/3** ya Mshahara wake kwa Mwezi.
- ✓ Mkopaji atalipa "**Service Charge**" **3%** na **Protection Fund 1% (sawa na 4%)**
- ✓ Lazima awe amejisajili katika mfumo wa Hazina Portal
- ✓ Mtumishi haruhusiwi kukopeshwa Mkopo mwingine kabla ya kurejesha Mkopo wa awali.
- ✓ Fedha za Mkopo zinalipwa kuitia Akaunti ya Mshahara
- ✓ Mikopo itatolewa kwa Watumishi kwa kuzingatia upatikanaji wa Mgao wa Fedha kutoka Hazina.
- ✓ Mtumishi lazima awe amethibitishwa kazini
- ✓ Waombaji ambao hawatafanikiwa katika mgao huu watakuwa kwenye Kanzi data ya Hazina na watapewa kipaumbele kwenye Mgao ujao.
- ✓ Mikopo hii inazingatia utaratibu wa **FIFO (First in – First Out)**, hivyo waombaji wa mwanzo ndio watakaopata kipaumbele na kazi hiyo inafanywa na Mfumo.

## B. Utaratibu wa kurejesha Mkopo

Mtumishi wa Serikali aliyenufaika kwa Mkopo wa Advances Fund, Makato yake yanakatwa kuitia Mshahara wake kila mwisho wa mwezi kuitia Mfumo wa utunzaji wa Kumbukumbu za Mishahara ya Watumishi (**HCMIS**).

**NB: Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 21/03/2025 saa 9:30 alasiri.**



Agape P. Fue

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

PANGANI.

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
(W) PANGANI